# KUMJUA MUNGU

## Darasa la 5
### la watoto

www.nuruyaupendo.com

by Denis & Devis Julius



# KUMJUA MUNGU NA KUTEMBEA KATIKA UWEPO WAKE.

Huu ni mwendelezo wa madarasa ya watoto. Ikiwa bado hujapata madarasa ya nyuma, basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo mwisho wa makala hii, ili tuweze kukutumia. Leo katika darasa hili jipya, Watoto watajifunza, Mungu hasaa ni nani. Hii itawasaidia wakati wote wawazapo, au wafikiripo juu ya Mungu wasiwe na mtazamo usio sahihi, Huu ni msingi mkubwa sana kwao. Hivyo darasa hili likizingatiwa vema kwa watoto, ni daraja zuri la wao kukua katika misingi imara ya kiroho.

Mwisho wa darasa mtoto ataweza kutambua;

Mungu ameumba vitu vyote ikiwemo na yeye.
Mungu ni Baba yake, ambaye anampenda na kumjali
Kila aanzapo kuomba amtaje Mungu, kama Baba yake
Namna ya kuisikia sauti yake, na kumwimbia.

Umri : Miaka 4-7

**By Mch. Denis & Devis Julius.**

# ENEO LA KWANZA (1)

## Mungu kama Muumba.

Hatua ya kwanza:

**Mwl:** Awali ya yote utaanza kwa Kuwasalimia watoto, na kuomba pamoja nao maombi ya kufungua darasa lenu.

Hatua ya pili:

**Mwl:** Watoto watamsifu Mungu na kumwabudu, walau kwa dk 15

Tumia nyimbo za tenzi, nyimbo za kuabudu, mapambio au sifa:

Mfano unaweza andaa Tenzi No. 114, inayosema 'Bwana Mungu nashangaa kabisa' - Ni nzuri sana, kwasababu inaeleza uzuri wa uumbaji wa Mungu.

Utawafundisha na kuwaongoza watoto pia, kuimba kwa kuinua mikono, kupiga makofi, na kufurahi..

Hiyo inawajengea nidhani nzuri ya kiibada na ya kumweshimu Mungu tangu wakiwa wadogo.

Hatua ya Tatu:

**Mwl:** Utauliza swali watoto 'Mungu ni nani'? Kisha utasikiliza maoni yao wanasemaje..Kila mmoja akishatoa majibu yake.

Wakishamaliza ndipo utawaeleza sasa kwa lugha rahisi kuwa Mungu ni nani.

**Mwl: Mungu ni muumba na ni Baba.**

Utawaambia wafungue biblia,(Hata kama hawajui kusoma), waonyeshe ni wapi kwenye biblia imeandikwa hivyo, (Usiwaonyeshe kwenye simu). Hiyo itawasaidia kujenga nidhamu ya usomaji vitabu lakini pia itawasaidia kujua mahali vifungu mbalimbali vinapopatikana kwenye biblia.

*Mwanzo 1:1 Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.*

**Mwl:** Waelezee kwa lugha rahisi, Mungu ameumba jua, mwezi, nyota, mawingi, pamoja na wao. Kwa kurejea kitabu cha Mwanzo sura yote ya kwanza.

Ndio sasa unaanza kutumia picha, au michoro, kuwaonyesha siku zote za uumbaji jinsi Mungu alivyoanza kuumba tokea siku ya kwanza hadi ile ya sita.

Wafungulie na waambie..

**Siku ya kwanza:**

*Mwanzo 1:3 Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru.*

Waambie mchana ni kwa jua na usiku kwa mwezi, waambie ukizima taa ni nini unaona?

Watajibu: ni giza.
Waambie giza linaficha vitu viovu

Tumia mifano dhahiri: Ukiweza waingize kwenye chumba, kisha zima taa zote, uwaambie watoto mnaona nini? Waseme giza, Kisha washa taa uwaambie mnaona nini? Waseme Mwanga.

Wafundishe kukiri tafsiri yake kiroho: **Mungu ameumba nuru na Nuru ipo ndani yangu, ambaye ni Yesu.**

**Siku ya Pili:**

(Mwanzo 1:6-8)

Mungu anagawanya maji, Na kuumba anga.

Watoe nje kisha uwaambie Mungu ameumba anga zuri la bluu, Waulize watoto wanaona nini kwenye anga?

Watajibu: Mawingi, Ndege, ..

Wafundishe kukiri kwanini Mungu ameliumba hilo?:

JIBU: **Mungu ameumba anga kwa utukufu wake.**

**Siku ya Tatu:**

Mungu aliumba ardhi, mimea, miti
(Mwanzo 1:9-13)

Hapa pia Watoe nje, waambie kila mmoja aguse ardhi chini waokote kipande kidogo cha jiwe/ udongo, kisha waambie kila mmoja akachume tawi dogo la mti au ua.

Kisha Waulize: Kwanini Mungu ameumba vyote hivi?

Ukiri: Mungu aliifanya mimea na nchi nzuri kwa ajili yetu,

**Siku ya nne:**

Mungu aliumba Jua, Mwezi, na Nyota.
(Mwanzo 1: 14-19)

Watoe nje! Watazame jua, (Angalizo usiwaambie waliangalie moja kwa moja, bali waelekeze tu kule lilipo)

Waulize pia Ulishawahi kuona nyota usiku?

Watasema ndio.

Kwanini Mungu aliviumba, vyote hivi.

Ukiri: Mungu anatutaka na sisi tuwe nuru ya ulimwengu. Kwa matendo yetu mema.

**Siku ya Tano:**

Mungu aliumba samaki na ndege. (Mwanzo 1:20-22).

Waonyeshe michoro ya samaki,(kama hutakuwa na samaki halisi) kisha waulize ni ndege gani wanaowajua.

Watasema: Kunguru, kuku, njiwa, bata, n.k.

Waulize wanaliaje? Kila mtoto aigilize milio hiyo.

Kisha wafundishe ukiri.

"Mungu aliviumba viumbe hai kwa utukufu wake, pia tuvitawale".

**Siku ya sita:**

Mungu aliumba wanyama na mwanadamu.

Waulize: Je! Mwanadamu ni nani?
Jibu: mwanamume na mwanamke.

Waulize je! Anatofauti yoyote na wanyama wengine?
Watoto: Ndio

Ukiri: Ameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu

Waagize, kila mmoja atazame uso wa mwenzake.
Waulize: Unamwona nani?
Wajibu: Namwona Mungu ndani yako.

**Siku ya Saba:**

Mungu akaacha kazi yake, akastarehe.

Waambie kila mmoja aigize kama vile ameketi chini amepumzika.

Kisha waambie, hivyo ndivyo Mungu alivyofanya alipomaliza kuumbwa ulimwengu.

Wafundishe ukiri: Bwana anataka tuikumbuke sabato yake, kwa kuacha kazi na mambo yetu tukamwabudu.

**Ziada:**

**Mwl:** Waulize kila mmoja ni kipi ambacho wamekipenda katika uumbaji wa Mungu.

Waambie tena kwa msisitizo, wakiri: Mungu ameumba ulimwengu na ameniumba na mimi.

Andaa Igizo: (kisha likawasilishwe mbele ya kanisa)

Kwa mifano, mbalimbali.

Baadhi wachume matawi ya miti, na maua, waigilize sauti za wanyama, kama ng'ombe, kunguru, kuku, wengine wachukue maji kwenye vyombo, wengine walete panzi nje, wengine, watembee kama wanyama fulani kisha wawataje, wengine washikane mikono.

Waweke makundi saba: Kila kundi litoe igizo lake, kufuatana na siku ya uumbaji.

Ni mwisho wote waseme..NA MUNGU AKAONA YA KUWA NI VEMA.!!

**Mwisho wajipange Mstari:** Kisha killa mmoja apite ataje jina lake, kisha aseme 'Mungu ameniumba mimi kipekee'

**Mstari wa kukariri:** (Mwanzo 1:1 Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.)

## ENEO LA PILI:

### Mungu kama BABA

Mwl: Waambie Mungu sio tu ametuumba, lakini pia anataka tumjue kuwa yeye ni Baba, hivyo anatupenda ,

anatujali na anatusikia pale tunapotaka kuongea na yeye na pale tunapotaka kuwa karibu na yeye.

**Mafundisho ya msingi.**

Tunatakiwa tumuite Mungu, Baba au Abba, kama Bwana Yesu alivyomuita..(Mathayo 6:9; Warumi 8:15)

**Mwl:** Waambie Sikuzote Baba mwema, hupenda, hulinda, uhudumia, anahuruma na hufundisha,. Mungu anafanya yote hayo.

**Mwl:** Ikiwa Mungu ni Baba basi anataka tuzungumze na yeye kila siku katika maombi.

**Mwl:** Wafundishe kusema Mungu wewe ni 'Baba yangu ninakupenda'

**Maombi ya Mwisho.**

**Mwl:** Waambie watoto watulie kuzungumza na Baba yao wa mbinguni. Kisha waongoze kusema maneno haya:

*"Baba yangu,*
*Asante kwa kuumba ulimwengu, Asante kwa kuniumba mimi kwa mfano wako na sura yako. Asante kwa wewe kuwa Baba yangu, unayenipenda. Nami nakupenda. Maisha yangu ninayakabisha kwako nikutumikie wewe. Ninaomba katika jina la Yesu Amen."*

Vifungu vya kukumbuka:

*Zaburi 103:13 Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, Ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao.*

***Mwisho***

**Kwa Mawasiliano:**

Kanisa la Nuru ya Upendo wa Kristo.
+255693036618 / +255789001312
www.nuruyaupendo.com
Email. info@wingulamashahidi.org